

**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam
2 Februari 2008**

Waliohudhuria

Aseli Wilison
Bushira Yahaya Rashidi
Dominata Rwechungura
Elaine Baker
Filbert Mbecha
Juma Ali Salehe Jongo
Jumanne Idd Selemani
Paulo Atibu Hatibu
Rashidi Saidi Karanji
Yusufu Juma

Mkutano na Wizara wa Miundombinu

Mejah, Elaine, Juma na Rashid walienda kutana na idara ya usalama barabarani ya Wizara ya Miundombinu tarehe 14 Januari lakini tulipewa dakika 15 tu hata kama miadi ilikuwa ya saa moja. Idara hawajasikiliza vizuri maoni yetu na walisema kwa sababu sisi hatujasoma uhanisi wala sheria hatuwezi kuchangia mawazo. Baada ya mkutano Elaine aliandika repoti na Juma aliwapelekea kwa katibu wa idara ya usalama barabarani wizarni.

Chuo cha Taifa cha Usafirishaji

Semina ya usalama barabarani ya tarehe 19 Januari ilienda vizuri sana na wanachama 21 waliohudhuria walipenda sana na walijifunza vitu vingi. Wakati wa mkutano wanachama walisema ni muhimu kutekeleza vitu ambavyo tumesoma kule. Tunatumaini kuendelea kushirikiana na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji. Elaine aliandia reporti na Juma alimpa Mr Wemba. Pia chuo walitupa kalenda kwa ajili ya ofisi yetu.

Barabara ya Morogoro

Tulizungumza kuhusu michoro ya barabara ya Morogoro. Wanachama walikuwa na mawazo haya :

- Kwa ujumla mipango yanatoa kipau mbele kwa wapanda baisikeli, na ina sehemu maalum ya wapanda baisikeli tofauti ya sehemu ya watembea kwa miguu kwenye stretches karibu zote
- Kwenye stretch 2 na stretch 10 (Mtaa Msimbazi) hakuna sehemu maalum ya baisikeli kwa sababu ya upotevu wa nafasi. Kwenye stretches hizi tunahitaji kujua baisikeli zitapita kwenye barabara ya magari au ya mabasi au ya watembea kwa miguu.
- Kwenye stretches zote ni muhimu kwamba baisikeli za walemavu na maguta pia wanaweza kuingia sehemu ya baisikeli. Vizuio kama nondo ambazo zinalinda sehemu ya baisikeli ziwe pana ya kutosha kwa maguta na baisikeli za walemavu kupita.

- Kwenye stretch 4 na stretch 5 inaonekana kuna mfereji / mtalo na miti kati ya sehemu ya baisikeli na barabara ya magari, kitu ambacho ni nzuri. Lakini kwenye stretches zingine (3, 6, 7, 8, 9) hatuna hakika kama kuna kitu chochote kati ya sehemu ya baisikeli na sehemu ya magari kuwalinda wapanda baisikeli. Inawezekana kwamba magari watatumia sehemu ya baisikeli kama sehemu ya parking au kupita foleni, basi tunapendekeza ziwe na vizio vya kuzuia magari kufanya hivi.
- Tunapenda kujua vipi magari yataingia kwenye plot, na wakati wanaingia kwenye plot kama wataweza kuingia kwenye sehemu ya baisikeli pia, au kama zitakuwa na vizio kama nondo kuzuia magari kuingia nija ya baisikeli wakati wanaingia plots.
- Tunapenda kuwa na taarifa kwamba ni shirika gani la serekali linahusika na taa mtaani na miti
- Tunapendekeza kwamba alama zionyeshe vizuri baisikeli zipite wapi na ziende kwenye direction gani

Elaine ataandika barua kwenda Halmashauri la Jiji na maoni haya.

Guta, ofisi na mambo ya hela

Ally Saidi Mwishehe alituma Tsh 7,000 kwenye mkutano huu na pia kwenye mikutano za wiki za nyuma.

Tuliamua kuwa na lengo la kufanya ufunguzi wa ofisi mwezi wa Machi. Kwa ajili ya hiyo lazima Ally Saidi Mohammed amalize bao za tangazo, na Elaine afanye printing ya taarifa zaidi. Juma pia alipendekeza tuwe na bao kwenye rafu kusaidia karatasi zisimame vizure. Aseli alipendekeza tuangalie jinsi ya kuzuia vumbi.

Tulikubali kununua helmeti, jaketi za njano na t-shirts ili zitumikwe kwenye ufunguzi na zitolewe kwa wanachama wakati wa ufunguzi. Tutachukua hela kutoka benki wiki hii kwa ajili ya hiyo na Mejah na Juma watanunua helmeti pamoja Ijumaa.

Kwa sasa Juma na Elaine wana Tsh 36,000 ya hela ya UWABA– walikuwa na chenji baada ya kuchukua Tsh 50,000 kwa ajili ya daftari na kalama na chai ya asubuhi ya semina, kuna hela ya guta na Juma amelipwa posho ya mwezi wa Januari.

Tawi

Tulikubali kwamba UWABA tufungue tawi Temeke. Wakati Elaine anarudi kutoka safari tunafanya mpango zaidi.

Sheria za barabara

Nakala ya Road Traffic Act na marekebisho yake sasa zipo ofisini kwenye rafu. Bado hatujapata regulations au sheria ndogo.

Nyinginezo

Jumanne na Bushira walipata ajali wakati wa kuendesha piki piki na waliumizwa miguu na mikono, lakini wanapona sasa. Dala dala ilifanya kosa lakini haijasimama wala kutoa repoti polisi. Jumanne alisema kwa sababu alivaa helmeti kichwa hakijaumizwa lakini bila helmeti angeumizwa sana, an alisema ni muhimu sana tuvae helmeti wakati wa kupanda baisikeli za kawaida pia.

Majibu ambayo bado hatujapata: Halmashauri la Jiji, Polisi wa Trafiki, Umoja wa Ulaya